



## Hakika Allah na Mtume wake ameharamisha kuuza pombe, na mzoga na nguruwe na masanamu

Kutoka kwa Jabiri bin Abdillah radhi za Allah ziwe juu yao na baba yake, yakwamba ye ye alimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akisema siku ya ufunguzi wa mji wa Makka, akiwa Makka: "Hakika Allah na Mtume wake ameharamisha kuuza pombe, na mzoga na nguruwe na masanamu", Wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wasemaje kuhusu samli (mafuta ya wanyama), kwani hutumika kupaka boti, na hupakwa ngozi, na watu huyatumia kuwashaa taa? Akasema: "Hapana, hayo ni haramu", kisha baada ya hapo akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Mwenyezi Mungu awalaani Mayahudi, kwani Mwenyezi Mungu alipowaharamishia samli (mafuta ya wanyama) waliyayeyusha, kisha wakayaauza, na wakala thamani yake".

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Jabiri bin Abdillah Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, alimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisema katika mwaka wa ufunguzi akiwa Makka: Hakika Mwenyezi Mungu na Mtume wake amekataza kuuza pombe, na mzoga na nguruwe na masanamu, wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je inajuzu kwetu kuuza mafuta ya wanyama waliokufa? Kwa sababu yanatumika kupaka boti (Mitumbwi), na ngozi na watu huwashaa taa zao kwayo. Akasema: Hapana, kuyauza ni haramu, kisha akasema: Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi, Mwenyezi Mungu alipowaharamishia mafuta ya wanyama, waliyayeyusha, kisha wakayaauza na kula thamani yake.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4556>

